li

zi wa
hatua
akula

bei za
gatia
uga-
aribu
ofisha
hiriki
hini.
18/19
unua
rama
kati-
bei
a juu
atika

## Kwa Ufupi

### Sekta za mifugo, uvuvi zatengewa Sh250 mil

Dodoma. Jiji la Dodoma limetenga Sh250 milioni kwa ajili ya idara ya mifugo na uvuvi pamoja na ujenzi wa miundombinu katika minada mitano.

Fedha hizo za mapato ya ndani zilipitishwa katika kikao cha bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 cha baraza la madiwani jijini hapa kilichofanyika hivi karibuni.

Katika kikao hicho Mkurugenzi wa jiji la Dodoma, Godwin Kunambi alisema minada ambayo watajenga miundombinu ya vijiwe vya kuchinjia na vyoo ni mnada wa Kikombo, Mbalawala, Mpunguzi, Msalato na Vikonje.

Hata hivyo, alisema katika fedha hizo Sh80 milioni ni kwa ajili ya kujenga machinjio ya kisasa ya nguruwe katika Kata ya Kizota ili kuboresha ubora na usafi wa nyama kwa afya ya walaji. Mkazi wa Dodoma Monica Malundo alisema uwepo wa shamba la malisho utapunguza changamoto ya wafugaji kuhangaika kutafuta malisho yaliyokuwa yakisababisha migogoro na wakulima.

(Nazael Mkiramweni)

### DC afafanua

Scanned with CamScanner

UAMUZI>> Hukumu ya kesi ya Zitto kusomwa Mei 29, mwaka huu.

# Kamati ya Mpina yafichua madudu kufuru

Na MWANDISHI WETU

KAMATI iliyoundwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina kuchunguza mradi wa ujenzi wa maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kituo cha Dar es Saalaam, imebaini ukikukwaji mkubwa wa sheria na usimamizi dhaifu.

Kutokana na hali hiyo, serikali imefanya uamuzi mgumu ikiwamo Waziri huyo kumuagiza Katibu Mkuu anayeshughulikia Uvuvi kutengua uteuzi wa Meneja wa Mradi wa Swiofish, Flora Luhanga kwa kushindwa kuusimamia.

Pia, ameagiza mkataba wa mshauri elekezi kurejewa upya kwa kubadili kiasi cha fedha kilichowekwa ambacho ni sh. milioni 600 badala ya sh. bilioni 1.2 iliyopo kwenye mkataba wa sasa na kurejesha fedha za ziada alizolipwa kiasi cha sh. milioni 352.

Kutokana na ripoti hiyo, Waziri Mpina aliagiza uchunguzi zaidi wa vyombo vya dola ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ufanyike ili kujua ni kwa jinsi gani ukiukwaji huo mkubwa ulifanyika na kuonya kuwa fedha za umma haziwezi tena kutumika vibaya katika miradi inayotekelezwa kwenye wizara yake.

Kwa mujibu wa taarifa ya wizara hiyo iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, Waziri Mpina ameagiza mkandarasi akatwe fedha zote kwa mkupuo kwa malipo yanayofuata ya sh. milioni 568 kwa kushindwa kuhuisha dhamana yake ya malipo ya awali na dhamana ya utekelezaji wa mradi.

Pia, mkandarasi ametakiwa kulipa sh. milioni 2.6 kila siku kutokana na kushindwa kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba kuanzia Aprili 21, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Waziri Mpina ametaka kiasi kitakachookolewa katika mradi huo cha zaidi ya sh. milioni 500 kipangiwe matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu muhimu ya makao makuu ya TAFIRI.

Akiwasilisha ripoti ya Kamati ya uchunguzi mbele ya Waziri Mpina, Kunduchi jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uvuvi, Magesa Bulayi, alisema kamati hiyo imebaini ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni katika kumpata mkandarasi na mshauri elekezi.

Bulayi alisema kamati hiyo ilihusisha watalaamu wabobezi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema kamati ilibaini pia kampuni iliyopewa kazi ya ujenzi ilipewa kazi hiyo yenye thamani ya sh. bilioni 2.6 huku ikiwa haina uwezo wa kifedha

INAENDELEA UK. 6

HUZUNI

Scanned with CamScanner

sehemu ya taarifa hiyo.

(Picha na Jumanne Gude)

# Kamati ya Mpina yafichua madudu kufuru

**Inatoka Uk. 5**

...kifedha jambo ambalo mesababisha ujenzi wa mradi usuasua na kukamilika asilimia 5 tu ambapo kwa mujibu wa ikataba mradi huo ulitakiwa wa umekamilika Aprili 20, waka huu.

Kamati hiyo pia ilibaini kuwa hamana ya malipo ya awali na hamana ya utekelezaji wa mradi enye thamani ya sh. milioni 598 meisha muda wake tangu Machi ), mwaka huu na kampuni husika ijahuisha dhamana hizo.

Aidha, alisema kamati pia baini makosa ya ukokotoaji wa ejeshaji wa malipo ya awali mbapo hadi kufikia hati namba 4 ya malipo kiasi kilichokuwa kimelipwa kwa serikali ni sh. milioni 54 tu badala ya sh. milioni 135.

Bulayi alisema kamati pia ilibaini kwamba mkandarasi aliahidi kwa mdomo kuokoa zaidi ya sh. milioni 500 katika mradi huo jambo ambalo halikuwahi kuelezwa mahali popote wala kuanishwa maeneo ambayo fedha hizo zitaokolewa.

Alisema Kamati ilitilia mashaka bei ya mzabuni mfano sh. 800,000 za gharama ya kabati la kupachika kwa 'unit' iliongezewa 0 kwa wino wa bluu katika nakala halisi ya makadirio ya ujenzi (BOQ) na kusomeka sh. 8,000,000 kinyume cha sheria za ununuzi.

Pia, Kamati ilibaini mshauri mwekelezi aliyepewa kazi ya usanifu na usimamizi wa miradi ya maabara ya TAFIRI Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba za watumishi wa MPRU Tanga na jengo la utawala Mafia yenye thamani ya sh. bilioni 4.5 lakini gharama ya mtaalamu mshauri huyo ni sh. bilioni 1.2 sawa na asilimia 27.4.

Kamati ilibaini kuwa gharama hizo ni kubwa ikilinganishwa na viwango vya ukomo vilivyowekwa na Bodi ya Wahandisi na Bodi ya Usanifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) ambapo gharama za mshauri elekezi zinaanzia wastani wa asilimia 12.45 hadi asilimia 13.75 ya gharama za mradi, lakini mshauri katika mradi huo alipewa asilimia 27.4 tofauti na kiwango kinachoruhusiwa.

Bulayi alisema Kamati ya uchunguzi imeona gharama alizostahili kupewa mshauri elekezi huyo ni sh. milioni 601 badala ya sh. bilioni 1.2, hivyo gharama ya mkataba ulioingiwa ni zaidi ya sh. milioni 654 ikilinganishwa na mwongozo wa bodi.

Kamati ilibaini gharama hizo ni kubwa ikilinganishwa na hali ya soko na kutolea mifano miradi ya ujenzi wa soko la Ndugai, Stendi, Kituo cha kuegesha malori Nala na Kituo cha mapumziko Chinangali na Barabara za Mzunguko Dodoma chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia wenye thamani ya sh. bilioni 87.7 lakini gharama ya usanifu na usimamizi ni sh. bilioni 1.5 tu sawa na asilimia 1.7 ya gharama ya mradi.

Pia, kamati imebaini ukiukwaji mkubwa wa sheria ya ununuzi wa umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013, pia imeonesha kutozingatiwa kwa masharti yaliyowekwa katika zabuni na mikataba ambapo baadhi ya watumishi wanahusishwa na ukiukukwaji huo.

Kutokana na ripoti hiyo, Waziri Mpina aliagiza uchunguzi zaidi wa vyombo vya dola ufanyike ili kujua ni kwa jinsi gani ukiukwaji huo mkubwa ulifanyika na kuonya kuwa fedha za umma haziwezi kutumika vibaya katika miradi inayotekelezwa kwenye wizara yake.

Scanned with CamScanner

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilala, Glory Nkwera ambaye amekazia hukumu hiyo na

kuondoka nyumbani, hivyo ndoa ibaki kama ilivyo.

Alisema kuwa Odunga alitakiwa kuonesha sababu za msingi,

yake ilikafaa ombi hilo badala yake ikamtaka alipe kiasi hicho cha fedha ikiwa ni sehemu ya gharama za

ndoa kanisani na kupata cheti cha ndoa.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina akisisitiza jambo kwa Mkurugenzi wa Uvuvi, Magesa Bulayi (kulia), mara baada ya kupokea ripoti ya uchunguzi wa ujenzi wa Maabara ya Taasisi ya Uvuvi iliyoko Kunduchi, Dar es Salaam. Katikati ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Petra Construction Co. Limited, Basem Abughalyoun, inayojenga maabara hiyo. (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina akisisitiza jambo kwa Mkurugenzi wa Uvuvi, Magesa Bulayi (kulia), mara baada ya kupokea ripoti ya uchunguzi wa ujenzi wa Maabara ya Taasisi ya Uvuvi iliyoko Kunduchi, Dar es Salaam. Katikati ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Petra Construction Co. Limited, Basem Abughalyoun, inayojenga maabara hiyo.** (Na Mpigapicha Wetu)

# Kamati ya Mpina yaibua madudu ujenzi wa Maabara ya TAFIRI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI iliyoundwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina kuchunguza Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Kituo cha Dar es Saalaam imebaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria pamoja na usimamizi dhaifu katika mradi huo na kuilazimu Serikali kufanya maamuzi magumu kutokana na kasoro zilizobainika.

Hivyo Waziri Mpina amemuagiza Katibu Mkuu Uvuvi kutengua uteuzi wa Meneja wa Mradi wa Swiofish, Flora Luhanga kwa kushindwa kusimamia mradi huo, huku akiagiza mkataba wa mshauri elekezi Kampuni ya Y&P Architect Limited kurejewa upya kwa kubadili kiasi cha fedha kilichowekwa kwenye mkataba kuwa sh. milioni 600 badala ya sh. Bilioni 1.2 iliyopo kwenye mkataba wa sasa pamoja na kurejesha fedha za ziada alizolipwa kiasi cha sh. milioni 352.

Aidha aliagiza Mkandarasi Kampuni ya Petra Construction Limited akatwe fedha zote kwa mkupuo kwa malipo yanayofuata kiasi cha sh. milioni 568 kwa kushindwa kuhuisha dhamana yake ya malipo ya awali na dhamana ya utekelezaji wa mradi na kutakiwa kulipa sh. milioni 2.6 kila siku kutokana na kushindwa kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba kuanzia Aprili 21, 2020.

Pia ametaka kiasi kitakachookolewa katika mradi huo cha zaidi ya sh. milioni 500 kipangiwe matumizi mengine ya ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu mingine muhimu ya Makao makuu ya TAFIRI.

Akiwasilisha ripoti hiyo ya Kamati ya uchunguzi mbele ya Waziri Mpina, Kunduchi jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uvuvi, Magesa Bulayi alisema kamati hiyo imebaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria na Kanuni katika kumpata Mkandarasi Kampuni ya Petra Construction Company Limited na Mshauri Elekezi Kampuni ya Y&P Architect Limited.

Alisema Kamati hiyo iliyoundwa na Waziri Mpina ilihusisha watalaamu wabobezi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Hivyo Bulayi alisema Kamati ilibaini pia Kampuni ya Petra Construction Company Limited ilipewa kazi ya ujenzi wa mradi huo wenye thamani ya sh. bilioni 2.6 huku ikiwa haina uwezo wa kifedha jambo ambalo limesababisha ujenzi wa mradi huo kusuasua na kukamilika asilimia 65 tu ambapo kwa mujibu wa mkataba mradi huo ulitakiwa kuwa umekamilika Aprili 20, 2020.

Kamati hiyo pia ilibaini kuwa dhamana ya malipo ya awali na dhamana ya utekelezaji wa mradi zenye thamani ya sh. milioni 598 zimeisha muda wake tangu Machi 30, 2020 na Kampuni ya Petra Construction Company Limited haijahuisha dhamana hizo.

Kamati pia ilibaini makosa ya ukokotoaji wa urejeshaji wa malipo ya awali ambapo hadi kufikia hati namba 4 ya malipo kiasi kilichokuwa kimelipwa kwa Serikali ni sh. milioni 54 tu badala ya sh. milioni 135.

Bulayi alisema Kamati pia ilibaini kwamba mkandarasi Kampuni ya Petra Construction Company Limited aliahidi kwa mdomo kuokoa zaidi ya milioni 500 katika mradi huo jambo ambalo halikuwahi kuelezwa mahali popote wala kuanishwa maeneo ambayo fedha hizo zitaokolewa.

Aidha Kamati ilitilia mashaka bei ya mzabuni mfano sh 800, 000 za unit price ya kabati la kupachika iliongezewa 0 kwa wino wa bluu katika nakala halisi ya makadirio ya ujenzi (BOQ) na kusomeka sh. 8, 000, 000 kinyume cha sheria za ununuzi.

Pia Kamati ilibaini Mshauri Mwekelezi Kampuni ya Y&P

**INAENDELEA UK. 5**

Scanned with CamScanner

changamoto za wachimbaji wadogo wa madini wilayani humo

# Kamati ya Mpina yaibua madudu ujenzi wa Maabara ya TAFIRI

Architect Limited iliyopewa kazi ya usanifu na usimamizi wa miradi ya Maabara ya TAFIRI Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba za watumishi wa MPRU Tanga na Jengo la Utawala Mafia yenye thamani ya sh. Bilioni 4.5 lakini gharama ya Mtaalamu Mshauri huyo ni sh. Bilioni 1.2 sawa na asilimia 27.4.

Kamati ilibaini kuwa gharama hizo ni kubwa ikilinganishwa na viwango vya ukomo vilivyowekwa na Bodi ya Wahandisi pamoja na Bodi ya Usanifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) ambapo gharama za Mshauri elekezi zinaanzia wastani wa asilimia 12.45 hadi asilimia 13.75 ya gharama za mradi lakini Kampuni ya Y&P ilipewa kwa asilimia 27.4 tofauti na kiwango kinachoruhusiwa.

Bulayi alisema Kamati ya uchunguzi imeona gharama alizostahili kupewa Y&P ni sh. milioni 601 badala ya sh. Bilioni 1.2 hivyo gharama ya mkataba ulioingiwa ni zaidi ya sh. milioni 654 ikilinganishwa na mwongozo wa bodi.

Kamati ilibaini gharama hizo ni kubwa ikilinganishwa na hali ya soko na kutolea mifano miradi ya ujenzi wa Soko la Ndugai, Stendi, Kituo cha kuegesha malori Nala na Kituo cha mapumziko Chinangali na Barabara za Mzunguko Dodoma chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia wenye thamani ya sh. Bilioni 87.7 lakini gharama ya usanifu na usimamizi ni sh. Bilioni 1.5 tu sawa na asilimia 1.7 ya gharama ya mradi.

Pia Kamati imebaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 pia imeonesha kutozingatiwa kwa masharti yaliyowekwa katika zabuni na mikataba ambapo baadhi ya watumishi wanahusishwa na ukiukukwaji huo.

Kufuatia ripoti hiyo, Waziri Mpina ameagiza uchunguzi zaidi wa vyombo vya dola ufanyike ili kujua ni kwa jinsi gani ukiukwaji huo mkubwa ulifanyika na kuonya kuwa fedha za umma haziwezi tena kutumika vibaya katika miradi inayotekelezwa kwenye wizara yake.

Kwa upande wao Mwakilishi wa Mkandarasi wa Kampuni ya Petra Construction Limited, Vallency Assenga alisema sababu za kuchelewa kujenga mradi huo ni mvua zinazoendelea pamoja na mlipuko wa Corona huku Mwakilishi wa Mshauri Mwelekezi Kampuni ya Y&P Architect, Anna Shayo alidai kuwa tayari alishamkumbusha kwa barua mkandarasi kuhuisha dhamana yake.

# Serikali yapunguza tozo usafirishaji samaki

SERIKALI imepunguza tozo mbalimbali za usafirishaji wa samaki na mazao yake ikiwemo kayabo, vichwa vya samaki na vifua.

Pia imefanya maboresho makubwa ya kanuni za uvuvi za mwaka 2009 ambayo yatajibu kwa upana changamoto za uvuvi, wavuvi na wadau wa uvuvi.

Hayo yalielezwa bungeni jijini Dodoma jana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wakati ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu,Maria Kangoye (CCM).

Katika swali lake,Kangoye alidai kumekuwa na changamoto nyingi katika uvuvi Ziwa Victoria, unaosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa uvuvi.

"Je Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inamaliza malalamiko haya,"aliuliza Kangoye.

Ikijibu swali hilo,Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ilieleza imepunguza tozo mbalimbali za usafirishaji wa samaki na mazao yake ikiwemo kayabo, vichwa vya samaki na vifua.

Pia, imefanya maboresho makubwa ya kanuni za uvuvi za mwaka 2009 ambayo yatajibu kwa upana changamoto za uvuvi, wavuvi na wadau wa uvuvi yanaendelea kufanyika ambapo yamewasilishwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Fedha kupata maoni yao kabla ya kukamilishwa.

Ilieleza wizara imekuwa ikishughulikia malalamiko, kero na matatizo ya wavuvi kwa kufanya vikao na mikutano na wavuvi pamoja na wadau wa uvuvi nchi nzima ili kuwasikiliza na kupata maelezo ya kina kuhusiana na malalamiko au matatizo yao.

Wizara imekuwa ikipokea malalamiko na matatizo ya wavuvi na wadau wa uvuvi hususan wa Kanda ya Ziwa Victoria kwa njia ya maandishi.

"Malalamiko mengi ya wavuvi na wadau wa uvuvi ukanda wa Ziwa Victoria yaliyokuwepo wakati wa Operesheni Sangara 2018, iliyolenga kupambana na uvuvi haramu, wizara imeyashughulikia kikamilifu na kuyatatua.

"Malalamiko makubwa yaliyoshughulikiwa ni pamoja na ukomo wa kuvua sangara wenye urefu wa sentimenta 85 ambapo uliondolewa, matumizi ya taa za sola,sasa zinaruhusiwa kwa kufanya marekebisho ya kanuni za uvuvi za mwaka 2009,"ilieleza wizara hiyo.

Mwendesha mkokoteni jijini Tanga, akiwa amepakia mizigo kupelekea gulio la Tangamano bila kuvaa barakoa za kujikinga na ugonjwa wa corona jana.

# JPM aombwa kuingilia kati mgogoro wa josho

**Na OSCAR ASSENGA**
-MUHEZA

RAIS Dk. John Magufuli, ameombwa kuingilia kati mgogoro ulioibuka baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na familia moja ya wanakijiji cha Kigombe ambao wanagombea umiliki wa josho la kuogeshea mifugo.

Wakati familia ya marehemu, Said Mwezema ikidai ndiyo mmiliki halali wa josho hilo kwa sababu lilijengwa mwaka 1988 na baba yao na lipo ndani ya shamba lao,huku Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, inadai lilijengwa na Serikali kati ya mwaka 1981 -82 na kuikabidhi Serikali ya Kijiji cha Kigombe kwa ajili ya usimamizi.

Wakizungumza jana viongozi wa familia ya Mwezema yenye makazi yake kijijini Kigombe, walisema josho ni mali yao kwa sababu lilijengwa mwaka 1988 na baba yao Said Mwezema aliyefariki dunia mwaka 2005 na lilikuwa likitumika kuogeshea ng'ombe wa familia pamoja na jirani.

Walisema wanashangaa kuitwa katika kikao kilichofanyika Aprili 22, mwaka huu kikiongozwa na Ofisa Mifugo,Christopher Sikombe pamoja na wataalamu kutoa idara mbalimbali, ikiwamo ya ardhi ambapo walifahamishwa rasmi josho hilo si mali yao tena, bali ni ya Serikali ya kijiji.

Ali Mwezema ambaye ni mdogo wa marehemu Said, alieleza kushangazwa kwake na kitendo cha halmashauri kudai josho hilo linamilikiwa na Serikali, wakati aliyejenga ni marehemu kaka yake mwaka 1988 na kwamba hata yeye alimsaidia kwa sababu alikuwa amerejea nyumbani kwa ajili ya likizo.

"Josho hili lilijengwa na kaka yangu,mimi nilimsaidia wakati niliporejea likizo ili ng'ombe wake na familia yetu waweze kuogeshwa hapo... nashangaa kusikia eti linamilikiwa na Serikali,"alisema Ali.

Mtoto mwingine wa marehemu, Akida Said alisema baada ya kufariki dunia baba yao, Serikali ilikarabati josho hilo kwa nyakati mbili tofauti bila makubaliano yoyote na familia.

"Baada ya baba kufariki, Serikali ililikarabati josho hili mara mbili tofauti bila ya kufanya makubaliano yoyote na familia,sasa hivi ndiyo tuseme Serikali ndiyo imejimilikisha kwa namna hii?" alihoji.

Alisema familia haitaki kudhulumu ardhi kwa sababu dini yao ya Kiislamu haielekezi, pia haiko tayari kuona inadhulumiwa tena kwa kutumia mabavu.

Alisema madhara ambayo yanaweza kutokea, iwapo halmashauri itaamua kuchukua kwa mabavu josho hilo kuwa ni pamoja na mifugo kuharibu mashamba yao na ya wanakijiji wengine,lakini pia kuna hatari ya kuenezwa magonjwa yatokanayo na mifugo kutoka maeneo mbalimbali.

Waliishauri halmashauri kujenga josho eneo jingine linalomilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Kigombe ambalo halitakuwa na migogoro wala usumbufu kwa mifugo.

Mkuu wa Idara ya Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza,Dk. Christopher Sikombe alisema josho hilo ni mali ya Serikali

ambayo ililijenga kati ya mwaka 1981-82 na kuikabidhi Serikali ya Kijiji cha Kigombe kwa ajili ya kuhudumia mifugo ya jamii.

Aliiom a familia kuepuka mivutano na Serikali kwa sababu itarejesha nyuma maendeleo ya mifugo ya wakazi wa eneo hilo ambao wanategemea josho hilo.

hutengeneza k
kupambana na
Aliwataka
watoto wasizag
ikiwa ni kuwa
na ukatili wa
wawapo mitaar
" Serikali i
shule zote za
na vyuo ili
nyumbani
ugonjwa wa
kuwakinga na
vya ubakaji n
tutamkuta m
mitaani hatua
dhidi yako m
kumsimamia,"a
Mwenyekiti
Cha Mapindu
Gugu aliwatak
waliopo maen
kuvaa barako
atakaeshindwa
hatua kali za kis
dhidi yake.
Pia alisisit
atakayehisi dali
afike kituo ch
karibu naye kwa
vipimo.
Mwenyekiti
uhamasishaji
huo, Ofisa Ma
Rose Kimaro al
utachukua siku
nyumba kwa ny

# Ngombe 34 wafa kwa kunywa maji yenye sumu

Na Samson Chacha, Tarime

NG'OMBE 34 na kondoo mmoja, wamekufa baada ya kunywa maji yenye kemikali za sumu katika mgodi wa mchimbaji mdogo, Boniface Alex katika Kata ya Kemambo Nyamongo wilayani Tarime Mkoa wa Mara.

Mifugo hiyo ni mali ya Nega Mwita wa kata hiyo, na Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri alifika eneoo la tukio akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya na maofisa mifugo na mazingira.

Aliagiza mizoga hiyo, kuzikwa chini ya ulinzi ; na mgodi huo kusimamisha uchimbaji na uchenjuaji madini.

Msafiri alisema tukio la mifugo hiyo, kunywa maji yaliyokuwa yanatiririka kutoka shimo bwawa dogo la mgodi wa mchimbaji Alex, lilitokea Jumatatu wiki hii mchana wakati watoto wa Nega walipokuwa wakichunga mifugo yao zaidi ya 45 karibu na maeneo ya mgodi huo.

Alieleza kuwa shimo la maji machafu yenye kemikali, lilikuwa limebomoka na kusababisha maji yake kutiririka kuelekea bondeni na mifugo hao kunywa na kupata madhara, huku mifugo mingine ng'ombe 10 na kondoo wawili wakinusurika kunywa maji hayo na 34 na kondoo mmoja kufa.

Alisema jamii inatakiwa kuchukua tahadhari kuruhusu watoto kuchunga mifugo, kucheza na maji yanayotiririka kutoka migodini, kwani maji hayo yana madhara makubwa kwa viumbe hai kutokana na kuchanganyikana na kemikali zenye sumu ni hatari kwa matumizi.

Scanned with CamScanner

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (aliyeshika sahani) akikagua ubora wa mahindi yaliyohifadhiwa katika ghala la Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Shinyanga alipofanya ziara katika ghala hilo jana. (Na Mpigapicha Wetu).

# DC aagiza waliosababisha mapigano wakulima, wafugaji wakamatwe

**Na Mwandishi Maalumu, Kipatimu**

MKUU wa Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Christopher Ngubiagai amemwagiza Kamanda wa Polisi wa wilaya hiyo kuwasaka na kuwakamata watu waliohusika na mapigano kati ya wakulima na wafugaji eneo la Kandawale, Kilwa Kipatimu.

Agizo hilo amelitoa juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kandawale alipokwenda kusuluhisha mgogoro huo unaotishia kuendelea kuvunjika kwa amani.

Aidha mkuu huyo wa wilaya amewataka wakulima na wafugaji katika wa kijiji hicho na wilaya nzima ya Kilwa, kuacha kujichukulia sheria mkononi na kama wanamalalamiko kuyafikisha katika mamlaka husika na sio kujichukulia sheria mkononi.

"Tiini sheria bila shuruti, anayekwenda kinyume mkondo wa sheria utakuchukua hatua zake" alisema Mkuu huyo wa wilaya.

Aidha ilielezwa katika mkutano huo kwamba pamoja na maboma kuunguzwa pikipiki moja pia iliunguzwa na watu kadhaa kujeruhiwa.

Akizungumza kama Mwenyekiti wa Kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, Ngubiagai alisema serikali haiwezi kuvumilia kuona raia wake wema wanateseka kwa sababu za watu kuoneshana ubabae.

"Hatuwezi kukaa na kuangalia watu wakikiuka sheria na kusababisha uvunjifu wa amani, aliyefanya hivyo ni lazima achukuliwe hatua," alisema Ngubiagai huku akionya dhidi ya vitendo vya ubabe vinavyofanywa na watu wanaodhani wana nguvu za kutawala wengine.

Aprili 20 mwaka huu katika kijiji cha Kandawale kulitokea mtifuano mkubwa kati ya wakulima na wafugaji na kupelekea mapigano kati yao na baadhi yao kujeruhiwa.

Alisema kitendo kilichofanywa cha kuondoa amani iliyopo katika eneo hilo hakiwezi kuvumiliwa iwe kimefanywa na mkulima au mfugaji.

Katika mkutano huo, baadhi ya wakulima walilalamika kwamba ndugu zao wafugaji wamekuwa kama mwiba katika miguu yao kutokana na vitendo vyao vya kifisadi ikiwamo kuingiza mifugo katika mashamba yao.

Aidha walisema tangu wamewakaribisha wafugaji wa kimang'ati katika eneo hilo, hali imechafuka sana, kutokana na wao kutumia uwezo wao kuwatisha wakulima na kusema kwamba hawawataki na wamewachoka.

Hata hivyo mmoja wa wafugaji, Juma Ngambishi aliitaka serikali kuona namna bora ya kuwasuluhisha kwani kitendo kilichofanywa na wakulima kuchoma maboma yao sio sahihi.

"Hata kama vijana walikuwa wameleta vurugu walikuwa wakamatwe na kushughulikiwa wao lakini si kwenda kuchoma moto maboma na kuharibu kila kitu na hata kuwapiga watu wasiohusika" alisema Ngambishi.

Mtendaji wa kijiji cha Kandawale alisema katika eneo hilo kulitokea vurugu mara mbili .

Vurugu ya kwanza ilitokea Aprili 7 na ya pili Aprili 20 na kusababisha kuita viongozi wa wilaya kwa kuwa hali ilikuwa tete.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo, vurugu zilianzishwa na vijana wa Kimang'ati waliokuwa katika sherehe katika eneo hilo walipoambiwa waondoke na kugoma wakidai kuibiwa unga wao.

Scanned with CamScanner

HABARI KITAIFA

# Kamati ya waziri yabaini madudu ujenzi maabara

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI iliyoundwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kuchunguza Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri) Kituo cha Dar es Saalam, imebaini ukiukwaji wa sheria na usimamizi dhaifu katika mradi huo.

Kutokana na kubainika kwa dosari hizo, Waziri Mpina amemwagiza Katibu Mkuu (Uvuvi) kutengua uteuzi wa Meneja wa Mradi wa Swiofish, Flora Luhanga, kwa kushindwa kusimamia mradi huo.

Waziri huyo pia ameagiza mkataba wa Mshauri Elekezi, Kampuni ya Y&P Architect Limited, kurejewa upya kwa kubadili kiasi cha fedha kilichowekwa kwenye mkataba kuwa Sh. milioni 600 badala ya Sh. bilioni 1.2 iliyoko kwenye mkataba wa sasa pamoja na kurejesha fedha za ziada alizolipwa kiasi cha Sh. milioni 352.

Vilevile, Mpina ameagiza Mkandarasi Kampuni ya Petra Construction Limited akatwe fedha zote kwa mkupuo kwa malipo yanayofuata kiasi cha Sh. milioni 568 kwa kushindwa kuhuisha dhamana yake ya malipo ya awali na dhamana ya utekelezaji wa mradi na kutakiwa kulipa Sh. milioni 2.6 kila siku kutokana na kushindwa kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba kuanzia Aprili 21 mwaka huu.

Mtaalamu huyo wa uchumi pia ameagiza kiasi kitakachookolewa katika mradi huo cha zaidi ya Sh. milioni 500, kipangiwe matumizi mengine ya ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu mingine muhimu ya makao makuu ya Tafiri.

Akiwasilisha ripoti hiyo ya Kamati ya Uchunguzi mbele ya Waziri Mpina Kunduchi jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uvuvi, Magesa Bulayi, alisema kamati hiyo imebaini ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni katika kumpata mkandarasi, Kampuni ya Petra Construction Company Limited na Mshauri Elekezi, Kampuni ya Y&P Architect Limited.

Alisema kamati hiyo iliyoundwa na Waziri Mpina, ilihusisha wataalamu wabobezi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Bulayi alisema kamati ilibaini Kampuni ya Petra Construction Company Limited ilipewa kazi ya ujenzi wa mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 2.6 huku ikiwa haina uwezo wa kifedha jambo ambalo limesababisha ujenzi wa mradi huo kusuasua na kukamilika asilimia 65 tu ambapo kwa mujibu wa mkataba mradi huo ulitakiwa kuwa umekamilika Aprili 20, mwaka huu.

Kamati hiyo pia ilibaini kuwa dhamana ya malipo ya awali na dhamana ya utekelezaji wa mradi zenye thamani ya Sh. milioni 598 zimeisha muda wake tangu Machi 30 mwaka huu na Kampuni ya Petra Construction Company Limited haijahuisha dhamana hizo.

Kamati pia ilibaini makosa ya ukokotoaji wa urejeshaji wa malipo ya awali ambapo hadi kufikia hati Na. 4 ya malipo kiasi kilichokuwa kimelipwa kwa serikali ni Sh. milioni 54 tu badala ya Sh. milioni 135.

Bulayi alisema kamati hiyo pia ilibaini mkandarasi, Kampuni ya Petra Construction Company Limited, aliahidi kwa mdomo kuokoa zaidi ya milioni 500 katika mradi huo jambo ambalo halikuwahi kuelezwa mahali popote wala kuainishwa maeneo ambayo fedha hizo zitaokolewa.

"Kamati ilitilia shaka bei ya mzabuni, mfano Sh. 800,000 za unit price ya kabati la kupachika iliongezewa '0' kwa wino wa bluu katika nakala halisi ya makadirio ya ujenzi (BOQ) na kusomeka Sh. 8,000,000 kinyume cha Sheria za Ununuzi.

"Kamati ilibaini Mshauri Mwekelezi, Kampuni ya Y&P Architect Limited, iliyopewa kazi ya usanifu na usimamizi wa miradi ya Maabara ya Tafiri Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba za watumishi wa MPRU Tanga na Jengo la Utawala Mafia yenye thamani ya Sh. bilioni 4.5, lakini gharama ya mtaalamu mshauri huyo ni Sh. bilioni 1.2, sawa na asilimia 27.4," alisema.

Aliongeza kuwa, kamati ilibaini gharama hizo ni kubwa ikilinganishwa na viwango vya ukomo vilivyowekwa na Bodi ya Wahandisi pamoja na Bodi ya Usanifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) ambapo gharama za mshauri elekezi zinaanzia wastani wa asilimia 12.45 hadi asilimia 13.75 ya gharama za mradi, lakini Kampuni ya Y&P ilipewa kwa asilimia 27.4 tofauti na kiwango kinachoruhusiwa.

Bulayi alisema kamati ya uchunguzi imeona gharama alizostahili kupewa Y&P ni Sh. milioni 601 badala ya Sh. bilioni 1.2, hivyo gharama ya mkataba ulioingiwa ni zaidi ya Sh. milioni 654 kulinganishwa na mwongozo wa bodi.

Alisema kamati ilibaini gharama hizo ni kubwa kulinganishwa na hali ya soko na kutolea mifano miradi ya ujenzi wa Soko la Ndugai, stendi, kituo cha kuegesha malori Nala na kituo cha mapumziko Chinangali na Barabara za Mzunguko Dodoma chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia wenye thamani ya Sh. bilioni 87.7, lakini gharama ya usanifu na usimamizi ni Sh. bilioni 1.5 tu, sawa na asilimia 1.7 ya gharama ya mradi.

Pia, alisema kamati imebaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013, akitolea mfano kutozingatiwa kwa masharti yaliyowekwa katika zabuni na mikataba ambapo baadhi ya watumishi wanahusishwa na ukiukwaji huo.

Scanned with CamScanner

TSB acting director-general, Saddy assets that had not yet been identified. with measures in the partner states pandemic.



Livestock and Fisheries minister Luhaga Mpina (2nd-L) inspects Tanzania Fishing Research Institute laboratory infrastructure yesterday. Others are TAFIRI director general Dr Ismael Kimerei (R) and Petra Construction Limited representative Nicholaus Mlay. Photo: Guardian Correspondent

Scanned with CamScanner

Aidha akahoji, ni kwa nini shule za serikali huwa

somo ya Kiswahili, sayansi, hisabati na sanaa zimesa-

Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso akijibu hoja za wabunge wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji, Bungeni jijini Dodoma juzi. (Picha na Mroki Mroki).

# Serikali kuendelea kutatua changamoto za usafirishaji samaki

SERIKALI imepunguza tozo mbalimbali za usafirishaji wa samaki na mazao yake ikiwemo kayabo, vichwa vya samaki na vifua.

Wizara wa Mifugo na Uvuvi ilitoa kauli hiyo bungeni jana wakati ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Maria Kangoye (CCM).

Kangoye alisema kumekuwa na changamoto nyingi katika uvuvi wa Ziwa Victoria unaosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa uvuvi. Na kuuliza serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inamaliza malalamiko hayo.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilijibu kwamba imekuwa ikishughulikia malalamiko, kero na matatizo ya wavuvi kwa kufanya vikao na mikutano na wavuvi pamoja na wadau wa uvuvi nchi nzima ili kuwasikiliza na kupata maelezo ya kina kuhusu malalamiko au matatizo yao.

Aidha, imekuwa ikipokea malalamiko/ kero na matatizo ya wavuvi na wadau wa uvuvi hususan wa Kanda ya Ziwa Victoria kwa njia ya maandishi.



Aidha, malalamiko mengi ya wavuvi na wadau wa uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria yaliyokuwepo wakati wa Operesheni Sangara 2018 iliyolenga kupambana na uvuvi haramu wizara imeyashughulikia kikamilifu na kuyatatua.

Aidha, malalamiko makubwa yaliyo shughulikiwa ni pamoja na ukomo wa kuvua sangara wenye urefu wa sentimeta 85 ambapo ukomo uliondolewa, matumizi ya taa za umeme wa jua ambapo sasa zinaruhusiwa kwa kufanya marekebisho ya kanuni za uvuvi za mwaka 2009.

Pia serikali imepunguza tozo mbalimbali za usafirishaji wa samaki na mazao yake ikiwemo kayabo, vichwa vya samaki na vifua. Vilevile, maboresho makubwa ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 ambayo yatajibu kwa upana changamoto za uvuvi, wavuvi na wadau wa uvuvi yanaendelea kufanyika.